**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**DODOMA**

**2024**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu :**
**Mkuu wa Shule: 0620418413/0752179863**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0629266588/0757001301**
**Matron/Patron:0747020354/ 0693728871**
**Shule ya Sekondari: HAMZA AZIZI ALLY MEMORIAL SECONDARY SCHOOL**
**S.L.P: 265 - NZEGA**
**Tarehe : 14-04-2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI HAMZA AZIZI ALLY MEMORIAL ,HALMASHAURI YA WILAYA NZEGA, MKOA TABORA, MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya PCM/PCB

Shule ipo kaskazini mwa mji wa Nzega barabara iendayo Shinyanga au Mwanza, kutoka Nzega mjini ni kilometa 29 hadi shuleni,aidha kutoka standi mpya ya mabasi kuna gari zinazokuja moja kwa moja kwa gharama ya Tshs 4,000/-,ila ukishukia njia panda kituo kilichopo katikati ya kijiji cha Nata na Nzegandogo iwapo utachukua bodaboda (pikipiki) ni Tshs 4,000/- au gari ni Tshs 1,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30/06/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 07/07/2024.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia: Sare za Shule**

i. Shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mirefu, suruali mbili (2) nyeusi zenye malinda mawili kila upande. (**ZISIZOBANA"model**") na tai mbili (2) nyeusi. **Zitakaguliwa**

ii. Soksi nyeusi ndefu pair 2

iii. Aje amevaa suruali ya Dark Blue **zenye malinda mawili kila upande** na shati la shule (**ambazo hazibani** ).

iv. Sare ya Michezo ni Track suit jozi mbili (02) rangi ya Dark Blue

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

viii. Sweta la rangi ya dark blue ;

ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) Tshirt (02) rang dark blue na suruali (02) dark blue

x. Tai mbili (02) za rangi nyeusi

xi. Tisheti (1) (T-shirt) rangi ya dark blue.

**2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari makubwa (counterbooks quire 3) yasiyopungua sita (06)

ii. **Ream (A4)** ya karatasi Mbili (2) kwa mwaka

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*PCB au PCM*);

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator;

vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe la sponji futi $2^1/_2$ .

vii. Mashuka ya rangi ya bluu Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 ya rangi ya blue ya $3^1/_2$

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. Mopa 1, Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

## 2.2 Michango mbalimbali

**Shule ya Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote lipia kwa akaunti ya shule AKAUNTI NAMBA 51102301499 Jina la akaunti ni SELF RELIANCE HAMZA AZIZI ALLY MEMORIAL SECONDARY SCHOOL**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ..................................................

**Jina la Mkuu wa Shule :GODFREY NASSORO JAPHARY**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ..................................................

THE HEADMASTER
HAMZA AZIZ ALLY MEMORIAL
SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 265, NZEGA
TABORA

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0620418413/ 0752179863**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0629266588/ 0757001301**
- **Mwandamizi Taaluma : 0626313643/ 0764964927**
- **Mwandamizi Malezi : 0747020354/ 0693728871**

**FORM NO.1**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA**

**SHULE YA SEKONDARI HAMZA AZIZI ALLY MEMORIAL**

---

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a government medical officer and returned to the Headmaster Hamza Azizi Ally Secondary school)

NAME.........................................................................................................

(Please examine the student named above and comment on his or her health recording to the following items. Kindly put a tick in out of either YES or NO whichever is applicable)

1. Does the student have problem in connection with

A: Sight?.........................................................................................1.NO..............
If YES state.....................................................................................2.YES.............

B:Hearing?......................................................................................1.NO..............
If YES state.....................................................................................2.YES.............

C: TB..............................................................................................1.NO.............
If YES state.....................................................................................2.YES............

D: Blood pressure...........................................................................1.NO.............
If YES state.....................................................................................2.YES............

E: Any other Health problems.........................................................1.NO............
If YES state.......................................................................................2.YES...........

F:Syphilis and other veneral diseases .........................................1.NO............
If YES state.......................................................................................2.YES...........
I: No please state............................................................................................

Name and signature..........................................Designation............................
................................Date .............................. Official stamp

**FORM NO.2**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA**

**SHULE YA SEKONDARI HAMZA AZIZI ALLY MEMORIAL**

---

**TAARIFA YA MWANAFUNZI**

1.Jina la mwanafunzi………………………………………………….

2.Kabila………………………………………………………………………….

3.Tarehe ya kuzaliwa………………Mwezi………………Mwaka……..

4.Amezaliwa\ katika wilaya……………….Mkoa…………………..

5.Dini…………………Dhehebu…………………………

6.Jina la mzaz/mlezi……………………………………………….………..

7.Anuani ya mzazi

/mlezi……………………………….Kijiji……………..Tarafa……………Wilaya…………..Mkoa………

……………….

namba ya simu………………………………………

8.Kazi ya baba/mlezi…………………………………

9.Kazi ya mama………………………………………

10.Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unahitaji uangalizi uandikwe,taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha

Daktari)…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

11.Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu),anuani zao kamili na namba zao za simu

(a) Ndugu…………………………………………………uhusiano……………………….

(b)Ndugu…………………………………………………uhusiano………………………..

(c)Ndugu…………………………………………………uhusiano………………………

……………………………………….                    …………………………………………...

SAINI YA MWANAFUNZI                    SAINI YA MZAZI/MLEZI

TATEHE…………………………..                    TAREHE……………………………

**FORM 03**

**MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………….(jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumikia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya.Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote.Naahidi kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya mwanafunzi……………………………..

Tarehe……………………………………..

shahidi

jina kamili………………………………………………….

Saini…………………………….

Tarehe…………………………..

**FOMU NO. 4**

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi…………………………………………………(jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa ……………………………………………kidato cha………………………………nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia kijana wangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo.Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria,kanuni, kulipia Ada na michango ya shule na maelezo mengine yaliyotolewa na shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi………………………………………..

Anuani kamili…………………………………………………

Saini………………………………………..

Tarehe……………………………………………

**VITABU VYA TAHASUSI VINAVYOPENDEKEZWA**

## PHYSICS

- S. Chand's principle of Physics – Class XI & XII-
- Principle of Physics – Rogers Municaster
- Advanced level Physics –Nelkon & parker
- Principle of physics – Tom Duncan

## BIOLOGY

- Advanced Biology for Secondary schools – (Michael R.), Biological science – (Taylor O J& Stoud G.W)
- Cell structure and organization – L. Msaki
- Understanding Biology – Fourth edition

## ADVANCED MATHEMATICS

- Advanced level mathematics – C. J TRANTER
- Pure Mathematics 1 & 2 – Backhouse
- Mathematics for A level ( volume 1 & 2) – S. Chand
- Advanced level Mathematics ( Vol 1) - L. K. Shayo

## CHEMISTRY

- Advanced level physical chemistry with General Chemistry – APE network 2012, 1 St Edition 2011
- Essential of Physical Chemistry – Arun Bahl
- Organic Chemistry – Arun Bahl, 1St Edition illustrative Reversed 2012

## GENERAL STUDIES

- General Studies for Advanced Level Certificate, Form five – Richard R.F Mbalase
- General Studies for Advanced Level Certificate, Form six – Richard R.F Mbasale

General Studies, supplementary book for advanced and collages, second edition -Konrad Adenaker S